



CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

MAFUNZO YA UJASIRIAMALI KWA WAHITIMU WA VYUO VYA ELIMU YA JUU “Badili Changamoto kuwa Fursa”

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anawatangazia wahitimu wote wa elimu ya juu kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeandaa mafunzo ya ujasiriamali yatakayotolewa katika jumla ya mikoa kumi ya Tanzania (mikoa nane Tanzania Bara na mikoa miwili Zanzibar) kuanzia mwezi Agosti hadi mwezi Oktoba mwaka 2019.

LENGO KUU LA MAFUNZO

Kuwapatia vijana uelewa, taarifa, maarifa, ujuzi na uwezo wa kuainisha fursa zinazowazunguka na kuweza kuzitumia fursa hizo kwa kuanzisha ajira kwa ajili yao na wenzao na hivyo kuboresha maisha ya jamii kwa ujumla.

MALENGO MAHUSUSI

- Kujenga uwezo na tabia ya kuona matatizo na changamoto kama fursa zitokanazo na taaluma zao.
- Kukutana na kujifunza kutoka kwa wajasiriamali wazoefu kutoka kwenye sekta mbalimbali kama vile, kilimo, ufugaji, madini, viwanda na huduma.
- Kutengeneza mipango ya biashara ambayo itawasaidia kutafuta mitaji.
- Kuwaunganisha vijana wenye mawazo mazuri ya ujasiriamali na watoa huduma za kifedha, teknolojia, uatamizi, nk.

WALENGWA

Mafunzo haya yanawalenga **vijana** wahitimu wa Vyuo vya Elimu ya Juu wenye nia ya kujiajiri.

MUDA WA MAFUNZO

Mafunzo haya yatatolewa katika makundi ya watu wasiozidi 50 kwa darasa kwa muda wa siku tatu mfululizo.

RATIBA YA MAFUNZO

Mahali	Tarehe za Mafunzo	Mwisho wa Kujisajili
Dar es Salaam	19/08/2019 - 31/08/2019	12/08/2019
Lindi	26/08/2019 - 31/08/2019	19/08/2019
Unguja Kusini	26/08/2019 - 31/08/2019	19/08/2019
Pemba Kaskazini	26/08/2019 - 31/08/2019	19/08/2019
Arusha	02/09/2019 - 11/09/2019	26/08/2019
Mwanza	02/09/2019 - 11/09/2019	26/08/2019
Dodoma	16/09/2019 - 25/09/2019	09/09/2019
Mbeya	16/09/2019 - 21/09/2019	09/09/2019
Iringa	18/09/2019 - 20/09/2019	09/09/2019
Katavi	23/09/2019 - 25/09/2019	16/09/2019

GHARAMA ZA MAFUNZO

Washiriki hawatalipa ada. Wanaotoka mbali watajigharamia usafiri na malazi.

JINSI YA KUSHIRIKI

Jisajili kwa kutuma barua pepe kwenye anuani udiec@udsm.ac.tz na mariamn261@gmail.com Au WhatsApp no. 0736-443-502 ikiainisha:

- Majina yako na namba ya simu.
- Mkoa utakapohudhuria mafunzo.
- Ambatanisha nakala ya cheti cha kuhitimu masomo yako ya elimu ya juu.

“WAHI KUJIANDIKISHA NAFASI NI CHACHE”

Kwa Mawasiliano zaidi:

Mkurugenzi, Kitengo cha Ubunifu na Ujasiriamali (UDIEC)

S.L.P 110099 Dar es Salaam, Tel: +255-736-443-502; +255-758-461-028, Email: udiec@udsm.ac.tz.